# AMAZING TANZANIA

Toleo no. 3 | AGOSTI 2025




Utalii waongoza fedha za kigeni mwaka 2024/25-Uk. 1

CHAN ilivyochochea utalii Tanzania-Uk. 24

Waliozuia uhamaji wa Nyumbu wafungiwa mwaka mmoja-Uk. 7

# YALIYOMO




**01** Utalii waongoza fedha za kigeni mwaka 2024/25

**03** Tanzania yazindua mkakati wa kitaifa wa mikoko

**05** Maagizo ya Rais Samia kujenga Makumbusho Kongwa yaanza kutekelezwa.

**06** Serikali yasaini mikataba minne ya uwekezaji yenye thamani ya dola milioni 158.5

**07** Waliozuia uhamaji wa Nyumbu wafungiwa mwaka mmoja.

**09** Wakulyamba alitaka Jeshi la Uhifadhi kujiandaa kutekeleza DIRA 2050

**10** Serikali yaimarisha ulinzi wa urithi wa kabila la Wahadzabe

**11** Serikali yazuia mradi wa magadi soda Ziwa Natron.

**12** Tanzania yaingia mara mbili orodha ya viwanja vya ndege vyenye safarinyingi Afrik,  hii ina maana gani kwa taifa.

**14** KITANDULA: Makumbusho ya UDSM, Urithi wa Kitaaluma na Kitamaduni

**16** Serikali yakabidhi ndege nyuki mpya 17 kukabili wanyamapori wakali.

**18** SGR Uvinza-Msongati kufungua ukurasa mpya wa utalii wa tiba.

**20** Dkt. Chana ahimiza jitihada za haraka kukabiliana na uhalifu wa mazingira Afrika.

**24** CHAN ilivyochochea utalii Tanzania

**28** Dkt. Chana ahimiza ushirikiano kati ya Japan na nchi za Afrika.

**30** Hadithi ya milima miwili: lakini upi ndio watatu kwa urefu Tanzania?

**33** Kitandula avutiwa na utafiti wa Nyuki wadogo, Hofadhi Ziwa Duluti

**33** Waziri Chana akutana na Ujumbe kutoka Ubalozi wa Iran.




# UTALII WAONGOZA FEDHA ZA KIGENI MWAKA 2024/25

SEKTA ya utalii imeongoza kwa kuingiza fedha za kigeni nchini katika mwaka 2024/25, kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) zilizotolewa Agosti 5, 2025.

Takwimu hizo zinaonesha kuwa hadi Juni 30, 2025, sekta ya utalii iliingiza dola za Marekani bilioni 3.934, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10 ya mapato yaliyotokana na watalii wa kimataifa, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliopita.

Kwa mujibu wa BoT, sekta ya madini ilishika nafasi ya pili kwa kuingiza dola za Marekani bilioni 3.67 katika kipindi hicho.

**Chart 2.7.2: Exports of Goods and Services**




Source: Tanzania Revenue Authority and Bank of Tanzania computations

Note: p denotes provisional data

Akizungumzia mafanikio hayo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbasi anasema kuwa mafanikio ya sekta hiyo yamechangiwa na mikakati madhubuti ya kuitangaza Tanzania kimataifa kwa kutumia majukwaa mbalimbali.

"Ni mwaka ambao filamu ya Royal Tour iliendelea kuoneshwa kwenye televisheni zaidi ya 300 nchini Marekani kupitia mitandao mikubwa kama PBS. Pia filamu mpya ya Amazing Tanzania iliyomshirikisha Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, ilizinduliwa Beijing, China na baadaye Dar es Salaam Novemba 2024," anasema Dkt. Abbasi.

"Ni wazi kabisa kuwa mafanikio haya yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na ushiriki wa viongozi wakuu wa nchi, usimamizi thabiti wa wizara pamoja na mchango wa wadau mbalimbali waliojitokeza kuitangaza Tanzania katika maonesho ya kimataifa."

Dk Abbas anaongeza kuwa: "kama kuna jambo tutalisimamia mwaka huu ni kuja na mikakati zaidi. Tanzania inahitaji dola na sisi ndio namba moja kuleta fedha za kigeni nchini. Je tulale? Hapana. Ubunifu wetu hautakuwa na mwisho katika kuzileta fedha za kigeni," anasisitiza Dkt. Abbas.

BANK OF TANZANIA

MONTHLY
ECONOMIC
REVIEW

July 2025









# TANZANIA YAZINDUA MKAKATI WA TAIFA WA MIKOKO

TANZANIA imezindua Mkakati wa Taifa wa Usimamizi na Maendeleo ya Mikoko (2025-2035) ambao umelenga kulinda bioanuwai na kuchochea maendeleo ya uchumi wa bluu nchini.

Mkakati huo wa miaka 10 unatarajia kugharimu Sh bilioni 54.7 na unalenga kuhifadhi na kurejesha asilimia 60 ya mikoko iliyoharibiwa nchini.

Takwimu zinaonesha Tanzania ina zaidi ya hekta 158,000 za mikoko, ambapo Delta ya Rufiji pekee inahifadhi takriban nusu ya mikoko yote nchini.

Akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Uhifadhi wa Mikoko iliyokwenda sambamba na uzinduzi wa Mkakati huo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk Pindi Chana anasema kuwa Serikali haitavumilia uzembe wa utekelezaji wa mikakati inayotungwa kwa gharama kubwa bila kuleta matokeo kwa wananchi.

Hivyo, Dk Chana anazielekeza taasisi za Serikali, ikiwemo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), taasisi za utafiti na wadau wa maendeleo kuhakikisha zinatekeleza kwa kasi na kwa ufanisi Mkakati huo ili kulinda bioanuwai na kuchochea maendeleo ya uchumi wa buluu nchini.






Anasema mikoko ni kinga muhimu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi kama vile mmomonyoko wa fukwe, na pia ni chanzo cha fursa mpya za kiuchumi ikiwemo biashara ya kaboni, utalii wa mazingira, ufugaji wa samaki na nyuki.

Kwa upande wake, Kamishna wa Uhifadhi wa Misitu wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo, anasema mkakati huo umeandaliwa kwa ushirikiano na wadau wa mazingira na utakuwa nyenzo muhimu katika uhifadhi endelevu wa mikoko unafanyika kwa kushirikisha jamii na sekta binafsi.

Mashirika mengine yaliyoshiriki kutoa mchango wa kitaalamu, kifedha na wa kielimu ni pamoja na Muungano wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira (IUCN), Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Hifadhi za Baharini na Maeneo Tengefu (MPRU), Mtandao wa Uhifadhi wa Ukanda wa Pwani (Mwambao), Shirika la EarthLungs na Wetlands International.



# MAAGIZO YA RAIS SAMIA KUJENGA MAKUMBUSHO KONGWA YAANZA KUTEKELEZWA

**Na Mwandishi Wetu**



Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zimeanza utekelezaji wa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, la ujenzi wa Makumbusho ya Taifa wilayani Kongwa, mkoani Dodoma.

Agizo hilo lilitolewa na Rais Samia Agosti 10, 2025, wakati wa ibada ya mazishi ya kitaifa ya aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Job Ndugai, iliyofanyika katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma.

Rais Samia alielekeza kuwa makumbusho hayo yatakuwa kumbukumbu muhimu ya harakati za ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika na kielelezo cha mchango wa Tanzania katika historia hiyo.

Anasema kuwa eneo hilo linapaswa kuendelezwa kama kivutio cha utalii wa kihistoria, akibainisha kuwa Hayati Ndugai wakati wa uhai wake alikuwa miongoni mwa viongozi waliopaza sauti juu ya umuhimu wa kuanzishwa kwa makumbusho hayo.

Akizungumzia hatua ya utekelezaji wa agizo hilo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula anasema Kongwa ni eneo lenye umuhimu wa kipekee kihistoria, kwa kuwa ni mahali ambapo marais watano wa nchi za Kusini mwa Afrika waliwahi kuishi na kupata mafunzo ya ukombozi dhidi ya ukoloni.

“Wataalamu wetu wanapaswa kuandaa mkakati madhubuti wa kulifanya eneo hili kuwa kituo cha utalii endelevu na hifadhi ya kihistoria, kwa manufaa ya taifa letu na nchi nyingine ambazo zilitumia Kongwa kama kitovu cha harakati za ukombozi,” anasema Mhe. Kitandula.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Mhe. Mayeka Saimon Mayeka, alizishukuru wizara zote mbili kwa kuitikia agizo la Rais kwa haraka, akisema hatua hiyo ni muhimu katika kufungua fursa za utalii na utafiti wilayani humo.

“Makumbusho haya yatakuwa kivutio cha kitaifa na kimataifa na yataimarisha utalii wa kihistoria pamoja na uchumi wa eneo letu.”





# SERIKALI YASAINI MIKATABA MINNE YA UWEKEZAJI YENYE THAMANI YA DOLA MILIONI 158.5

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imesaini mikataba minne ya uwekezaji yenye thamani ya dola za Marekani milioni 158.5(sawa takribani Sh bilioni 403) kupitia mpango wa Uwekezaji Mahiri (SWICA).

Uwekezaji huo unahusisha vitalu vya Burko Open Area (Monduli- Arusha), Selous MHJ1, Selous MHJ2 na Selous ML1 (Liwale – Lindi) ambapo wawekezaji watakuwa na fursa ya kufanya shughuli za utalii wa picha na uwindaji wa kitalii ndani ya kitalu kimoja.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana anasema mpango huo unalenga kuleta tija zaidi katika sekta ya maliasili kwa kuvutia wawekezaji na kuongeza mapato ya Serikali.

"SWICA ni mfumo bunifu unaowezesha mwekezaji kutumia kitalu kwa shughuli mbalimbali za utalii badala ya uwindaji pekee, na hii ni tofauti na utaratibu wa uwindaji wa kitalii unaomtaka mwekezaji kwa kiasi kikubwa kufanya shughuli za uwindaji pekee. Hii ni njia bora ya kuimarisha uhifadhi na kuongeza faida kwa taifa."

Dk Chana anasema mikataba hiyo inatarajiwa kuiingizia Serikali dola za Marekani milioni 281.5 (sawa na Sh bilioni 719) kwa kipindi cha miaka 20, sawa na wastani wa Sh bilioni 36 kwa mwaka huku.

Pia wananchi wa vijiji vinavyozunguka maeneo ya uwekezaji watanufaika na ajira na miradi ya maendeleo ya jamii ikiwamo zahanati, maji madara ambayo itagharimu takribani dola za Marekani milioni 1.8 sawa na Sh bilioni 4.6

Mpango wa SWICA ni miongoni mwa jitihada za Serikali za kuvutia uwekezaji wa kimkakati kwenye sekta ya maliasili na utalii huku ukizingatia uhifadhi endelevu wa mazingira na ushirikishwaji wa wananchi katika maendeleo.






# WALIOZUIA UHAMAJI WA NYUMBU WAFUNGIWA MWAKA MMOJA

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) imewapiga marufuku kwa kipindi cha mwaka mmoja waongozaji watalii sita kwa kukiuka kanuni za hifadhi.

Waongozaji hao, ambao pia ni madereva wa safari kutoka kampuni za utalii, hawataruhusiwa kufanya kazi yoyote ya kitaalamu ndani ya hifadhi za taifa za Tanzania katika kipindi hicho.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA, Musa Kuji, waongozaji hao walikiuka maadili ya kitaalamu kwa kuwaruhusu watalii kushuka kwenye magari na kuziba eneo muhimu la kuvuka kwa makundi ya nyumbu katika eneo la Kogatende la Mto Mara ndani ya Hifadhi ya Serengeti.

Kitendo hicho kilisababisha mkanganyiko na taharuki miongoni mwa Wanyama na kwa baadhi ya matukio watalii waliruhusiwa hata kukaa juu ya magari.

Matukio hayo, yaliyotokea kati ya Julai 20 hadi 29, 2025, yalifichuliwa baada ya mwongozaji na mpigapicha wa wanyamapori kutoka Afrika Kusini, Nick Kleer kuposti video ya tukio hilo la kuziba njia ya nyumbu.

Waliokubwa na adhabu hiyo na kampuni zao kwenye mabano ni Tareto Samwel (Asilia Lodges & Camps Ltd), Lucas S. Manonga (L & L Tanzania Safaris Co. Ltd) na Edmund I. Burra (Nomad Tanzania Ltd) ambao walitenda kosa hilo Julai 21 mwaka huu.

Wengine ni Elidanos J. Tito (Lapwing Company Ltd) aliyetenda kosa Julai 24 mwaka huu, Richard A. Ngowi (R & R Tanzania Specialist Ltd) aliyetenda kosa Julai 25 mwaka huu Ombeni J. Mbise wa Africa Scenic Safaris Ltd aliyefanya kosa Julai 28 mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waendeshaji Utalii Tanzania (TATO), Bw. Elirehema Maturo amepongeza uamuzi wa TANAPA na kuongeza kuwa hatua hiyo itazuia ukiukaji wa sheria za uhifadhi wa wanyamapori katika siku zijazo.

“Hii ni hatua ya kupongezwa kutoka TANAPA na wadau wote wanapaswa kuiunga mkono,” anasema.

Anasema kuwa TATO imechapisha kijitabu cha Kanuni na Maadili ya Safari, ambacho kimetafsiriwa kwa lugha tisa, ili kuhamasisha utii wa sheria za uhifadhi miongoni mwa waongozaji wa safari na watalii.

Katika miaka ya hivi karibuni, TANAPA imeongeza doria, kuanzisha adhabu kali zaidi na kushirikiana kwa karibu na waendeshaji wa utalii kuwaelimisha watalii juu ya mwenendo bora wa safari.

Marufuku hiyo itadumu hadi katikati ya mwaka 2026, jambo ambalo linamaanisha kuwa madereva waliopigwa marufuku hawatashiriki msimu wa uhamiaji wa nyumbu wa mwaka ujao.



# WAKULYAMBA ALITAKA JESHI LA UHIFADHI KUJIANDAA KUTEKELEZA DIRA YA 2050

**Na Mwandishi Wetu**



TAASISI zinazounda Jeshi la Uhifadhi zimetakiwa kupitia na kujipanga kikamilifu kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 hususan kwenye maeneo ya uhifadhi wa urithi wa maliasili ikiwemo wanyamapori, misitu na malikale.

Rai hiyo imetolewa Arusha na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii anayeshughulikia Maliasili, CP. Mabula Wakulyamba wakati wa kikao kazi kati ya Wizara na taasisi za Jeshi la Uhifadhi kilicholenga kuwajengea uelewa wa pamoja wa uimarishaji wa uhifadhi endelevu wa maliasili kwa kuzingatia melekezo ya Tume ya Haki Jinai.

Anasema utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050 ni njia sahihi ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuleta maendeleo kwa wananchi na taifa kwa ujumla kupitia uhifadhi endelevu wa urithi wa maliasili.

"Tunayo dira ya maendeleo. Ni wajibu wa taasisi zote za Jeshi la Uhifadhi kuielewa, kuipitia na kujiandaa kuitekeleza ipasavyo. Hii ni sehemu ya mchango wetu katika maendeleo ya nchi."

Aidha, CP. Wakulyamba anasema pamoja na kuwa Jeshi hilo linafanya kazi nzuri, ni lazima taasisi zake zote zishirikiane na kuongeza nguvu katika ulinzi wa maliasili dhidi ya watu wachache wenye nia ovu dhidi ya rasilimali hizo huku akisisitiza matumizi ya tafiti za ndani kama nyenzo muhimu katika kutatua changamoto zilizopo kwenye sekta ya uhifadhi.

" Wizara inao wataalamu wabobezi kwenye nyanja za uhifadhi, utalii na malikali, ni muhimu tukatumia maarifa yao ya kitaaluma ili kuleta mabadiliko chanya."

Akizungumza kwa niaba ya Wakuu wa taasisi za Jeshi la Uhifadhi, Kamishna Mkuu wa Uhifadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dossantos Silayo ameahidi kusimamia vyema utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050, mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai na kusimamia nidhamu na uadikifu kwa askari wa Jeshi hilo.






# SERIKALI YAIMARISHA ULINZI WA URITHI WA KABILA LA WAHDZABE

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha, Dkt. Lameck Karanga amesema

Serikali imeanza kuchukua hatua dhidi ya raia wa kigeni na waongoza watalii wanaorekodi maudhui yasiyofaa kwa kabila la Wahadzabe.



Akizungumzia hatua hizo, Mkuu wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha, Dkt. Lameck Karanga anasema ofisi yake kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji imechukua hatua ya kuwahoji raia wa kigeni na kubaini haishi kihalali baada ya vibali kuisha muda wake.

“Tuliwakamata na kuwahoji na tumebaini hawaishi kihalali kwani vibali vimeisha muda wake na hatua stahiki dhidi yao zitachukuliwa.”

Dkt. Karanga anasema kwa waongoza watalii walioshiriki katika tukio hilo pia wamechukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufungiwa kupeleka watalii katika eneo la Wahadzabe lenye urithi adhimu na adimu wa kiutamaduni.



# SERIKALI YAZUIA MRADI WA MAGADI SODA ZIWA NATRON

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali imesisitiza kuwa hakuna leseni iliyotolewa, wala haitatolewa, kwa ajili ya uchimbaji wa magadi soda ndani ya Ziwa Natron, licha ya tafiti kuonyesha wingi wa rasilimali hiyo.

Hatua hiyo ni katika kulinda uhifadhi wa ZiwaNatron ambalo linatambulika kimataifa kupitia Mkataba wa Ramsar.

Ni eneo la oevu lenye umuhimu mkubwa kwa makazi ya ndege maji zaidi ya 100,000, samaki adimu aina ya Oreochromis alcalicus na mwani wa Spirulina platensis ambao ni chakula kikuu cha ndege jamii ya Flamingo.

Akizungumza kuhusu suala hilo, Naibu Waziri wa Madini, Stephen Kiruswa anasema eneo la Ziwa Natron liko chini ya mkataba wa Ramsar na linalindwa na Umoja wa Mataifa hivyo haliruhusiwi kwa uwekezaji wa aina yoyote kuchimba madini hayo.

“Shughuli pekee inayoruhusiwa ni uokotaji wa asili wa magadi pembezoni mwa ziwa,” anasema Mhe. Kiruswa.

Hata hivyo, Serikali imeelekeza kuwa kampuni zinazotaka kuwekeza katika magadi soda zishirikiane na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na kuelekeza shughuli hizo kufanyika eneo la Engaruka wilayani Monduli.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Nature Tanzania na Mtaalamu wa Ndege, Emmanuel Mgimwa anasema uchimbaji wa magadi soda katika Ziwa Natron utaathiri kwa haraka maisha ya Flamingo.

Idadi ya Flamingo duniani imeshuka kutoka milioni 4.5 hadi milioni 1.5 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na Tanzania ina zaidi ya asilimia 80 ya Flamingo waliobaki duniani.

Kupungua huko kunachangiwa na uharibifu wa makazi na maeneo yao ya kuzaliana.

Mgimwa anasema kuwa mradi wowote katika Ziwa Natron ungehitaji mabadiliko ya mito inayopeleka maji ziwani, ikiwemo Mto Ewaso Ng’iro kutoka Kenya, jambo ambalo litavuruga usawa wa maji unaohitajika kwa Flamingo kuzaliana.






# TANZANIA YAINGIA MARA MBILI ORODHA YA VIWANJA VYA NDEGE VYENYE SAFARI NYINGI AFRIKA: HII INAMAANA GANI KWA TAIFA

**Na Mwandishi Wetu**

Tanzania imeweka historia kwa kuingiza viwanja viwili vya ndege kwenye orodha ya viwanja 10 vinavyoongoza kwa safari nyinge za Afrika kufikia Julai 2025.

Viwanja hivyo ni uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA-ZNZ) ulishika nafasi ya tisa kwa kupokea wasatani wa safari 92 za ndege kwa siku, huku Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA-DAR) jijini Dar es Salaam ukishika nafasi ya kumi kwa safari 84 kwa siku.

Hatua hii inaifanya Tanzania kuungana na mataifa makubwa ya usafiri wa anga barani Afrika kama vile Afrika Kusini (Johannesburg) na Ethiopia (Addis Ababa).

Hatua hii imechochewa na ukuaji wa diplomasia ya utalii ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, hasa kupitia uzalishaji na usambazaji wa filamu ya The Royal Tour duniani kote na kwa yeye binafsi kukaribisha wageni kutembelea Tanzania kwa kutangaza hazina ya asili na tamaduni ya taifa kwenye jukwaa la kimataifa.

Matokeo yake ni ongezeko kubwa la uelewa wa kimataifa kuhusu Tanzania, jambo linachangia ongezeko la kihistoria la idadi ya watalii Zanzibar na Tanzania Bara, na hivyo kuongeza mahitaji ya safari za ndege na shughuli katika viwanja vya ndege.

Kutambuliwa kwa viwanja vya Zanzibar na Dar es Salaam kuwa miongoni mwa viwanja vyenye safari nyinge za ndege Afrika si tu suala la heshima, bali ni ishara ya ukuaji wa uchumi na kuimarika kwa mtandao wa kimataifa wa usafiri.

Kung'ara kwa Zanzibar kunadhihirisha hadhi yake kama eneo mojawapo lenye vivutio vya likizo vinavyoongoza Afrika, huku ongezeko la safari za ndege likiwa linamaanisha kuongezeka kwa watalii, mapato ya fedha za kigeni, na ajira kupitia sekta ya hoteli, usafiri na utamaduni.

Pia Dar es Salaam kama kitovu cha biashara cha nchi inanufaika na kuimarika kwa miunganisho ya safari zinazochochea usafirishaji wa mizigo, safari za kibiashara, na fursa za uwekezaji, hasa na nchi majirani za Afrika Mashariki na washirika wa kimataifa. Kwa pamoja, mafanikio haya yanaiimarisha Tanzania kama chapa ya taifa na kuibeba katika ramani ya dunia.

Nyuma ya mafanikio haya ipo Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ambayo ndiyo mdhibiti wa sekta ya usafiri wa anga nchini.

TCAA imehakikisha viwango vya kimataifa vya usalama na ulinzi vinafuatwa, imeboresha taratibu za utoaji wa leseni na ithibati kwa waendeshaji na kushirikiana na mamlaka za viwanja vya ndege na mashirika ya ndege ili kuhakikisha ukuaji endelevu.

Pia uendeshaji mashirika ya ndege, kampuni za huduma ardhini na wamiliki wa viwanja wamewekeza katika kuboresha huduma, kuongeza ndege na kuboresha huduma kwa wateja yote haya yakichangia kuifanya Tanzania kuwa kitovu kinachoinukia cha usafiri wa anga barani Afrika.

Kwa kuwa viwanja vya ndege vya Tanzania sasa vimeg'aa kwenye ramani ya anga ya Afrika, changamoto ni kuendeleza na kupanua mafanikio haya kwa kuwa na uwekezaji endelevu katika miundombinu ya viwanja vya ndege, kuitangaza Tanzania na ushirikiano madhubuti kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuongeza uwezo wa huduma kwa viwango vya kimataifa.

Hatua ya Tanzania kuingia mara mbili kwenye orodha ya viwanja 10 vyenye safari nyingi za ndege Afrika ni alama na ishara ya mafanikio ya taifa katika sekta ya anga, utalii na maendeleo ya uchumi na fursa nyingi zinazokuja.



# KITANDULA: MAKUMBUSHO YA UDSM, URITHI WA KITAALUMA NA KITAMADUNI

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula, amesema kuwa uzinduzi wa makumbusho maalum katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ni hatua muhimu katika kuhifadhi na kuenzi urithi wa kitaaluma, kitamaduni na kihistoria wa taifa.



Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo iliyofanyika chuoni hapo leo, Mhe. Kitandula anasema makumbusho hayo ni alama ya kudumu ya maendeleo ya elimu nchini, huku ikitoa fursa kwa wanafunzi, watafiti na wadau mbalimbali kuunganishwa moja kwa moja na historia ya kielimu ya UDSM na taifa kwa ujumla.

“Makumbusho haya yanafungua ukurasa mpya wa historia kwa kuhakikisha urithi huu muhimu unahifadhiwa, kuenziwa na kuwa chachu ya hamasa kwa vizazi vijavyo kufanikisha malengo makubwa zaidi ya kitaifa,” anasema Mhe. Kitandula.



Aidha, alibainisha kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii itaendelea kushirikiana kwa karibu na UDSM katika kuyatangaza makumbusho hayo kama kivutio cha utalii wa kiutamaduni na kielimu kwa watalii wa ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Balozi Mwanaidi Sinare Maajar, anasema makumbusho hayo yatakuwa jukwaa la kuwauunganisha wataalamu wa masuala ya uhifadhi kutoka ndani na nje ya Tanzania, hatua itakayosaidia kuimarisha tafiti na maonesho ya kihistoria na kitamaduni.

Awali, Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye anasema kuwa makumbusho hayo yatatumika kama darasa hai kwa vizazi cha sasa na vijavyo, na itachochea uelewa mpana kuhusu historia ya kitaaluma na utamaduni wa taifa.






# SERIKALI YAKABIDHI NDEGE NYUKI MPYA 17 KUKABILI WANYAMAPORI WAKALI

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imekabidhi ndege nyuki mpya 17 kwa Jeshi la Uhifadhi, zenye thamani ya Sh bilioni 1.14, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa doria za anga katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu nchini.

Makabidhiano hayo yalifanyika wakati wa hafla ya kufunga mafunzo maalum ya matumizi ya ndege hizo kwa maofisa na askari 84 kutoka Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).



Anasema kuwa ndege hizo zimenunuliwa na Serikali kupitia Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori (TWPF), ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuhakikisha usalama wa watu, mali na maliasili unadumishwa.

Aidha, Waziri Chana alitangaza kuanza kutumika rasmi kwa Mfumo wa Kidigitali wa Problem Animals Information System (PAIS), ambao utawezesha ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za matukio ya wanyamapori kwa ufanisi zaidi.



Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo (anayeshughulikia Maliasili), CP Benedict Wakulyamba, aliwataka wahitimu wa mafunzo hayo kuhakikisha wanavitunza vifaa hivyo ili viweze kutumika kwa ufanisi katika kudhibiti wanyamapori hatarishi na kuimarisha mapambano dhidi ya ujangili.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, Dkt. Alexander Lobora anasema kukabidhiwa kwa idadi kubwa ya ndege nyuki ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, alilolitoa wakati wa ziara yake katika mikoa ya kusini mwa Tanzania.

“Hili ni tukio la kihistoria katika juhudi za kulinda maliasili zetu. Tunamshukuru Rais kwa maono haya ya kimkakati,” anasema Dkt. Lobora.






# SGR UVINZA–MUSONGATI KUFUNGUA UKURASA MPYA WA UTALII WA TIBA




TANZANIA na Burundi zimeandika historia mpya ya ushirikiano wa kiuchumi na kijamii baada ya kuzindua rasmi ujenzi wa reli ya kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR) kutoka Uvinza, mkoani Kigoma hadi Musongati, nchini Burundi.

Hatua hiyo mbali na kurahisisha usafiri na biashara baina ya nchi hizo mbili jirani, bali itaibua kuibua fursa mpya ya utalii wa tiba unaoshika kasi duniani

Tayari matarajio hayo yameanza kuonekana wazi, kufuatia kliniki maalumu ya tiba iliyoendeshwa na wataalum kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Burundi, iliyofanyika hivi karibuni jijini Bujumbura.

Kambi hiyo ya kitabibu imeibua shauku kubwa kwa wananchi wa Burundi waliovutiwa na ubora wa huduma za afya kutoka Tanzania, na hivyo kuibua mahitaji mapya ya usafiri wa uhakika kufika hospitali za kisasa kama Benjamin Mkapa na Muhimbili.




Reli hiyo pia inakwenda kukuza utalii kati ya nchi hizo, hivyo kuongeza watalii kutoka Burundi watakaofika Tanzania kushuhudia vivutio mbalimbali vya asili vya utalii.

Tanzania inatajwa kuwa kitovu cha idadi kubwa ya simba barani Afrika, pamoja na wanyamapori wakubwa kama tembo, twiga, na faru, vivutio ambavyo havipatikani nchini Burundi.

Kwa kuimarika kwa miundombinu ya reli, inatarajiwa sasa kuwa ni rahisi zaidi kwa wageni kutoka Burundi kufika katika hifadhi mbalimbali kama Serengeti, Mikumi, na Ruaha bila vikwazo vya usafiri.

Hafla ya uzinduzi na uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa reli ulihudhuriwa na viongozi wakuu wa nchi hizo mbili ambao ni Rais wa Burundi, Mheshimiwa Meja Jenerali Évariste Ndayishimiye na Waziri Mkuu wa Tanzania Kassim Majaliwa, aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Aidha, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, alimwakilisha Waziri wa Wizara hiyo, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana.





# DKT. CHANA AHIMIZA JITIHADA ZA HARAKA KUKABILIANA NA UHALIFU WA MAZINGIRA AFRIKA

RAIS wa Baraza la Uongozi la Mkataba wa Lusaka (LATF) na Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dkt. Pindi Chana amezitaka serikali za Afrika, Japani, wadau wa maendeleo na sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya kidijitali ya uhifadhi

Hatua hiyo itasaidia itaharakisha katika kukabiliana na uhalifu wa mazingira barani Afrika.

Dr. Chana ametoa wito huo jijini Yokohama, Japani, katika mjadala kuhusu mageuzi ya Vituo vya Kamandi na Udhibiti vya Kikanda na Miundombinu ya Umma ya Kidijitali (DPI) katika kukabiliana na changamoto za migogoro ya asili ya binadamu barani Afrika.

“Natoa wito kwa serikali duniani kuunga mkono maono ya Kikosi Kazi cha Makubaliano ya Lusaka ya kuanzisha Kituo cha Uongozi na Udhibiti wa Kikanda pamoja na Miundombinu ya Umma ya Kidijitali. Huu ni uwekezaji si tu kwa ajili ya kulinda bayoanuwai, bali pia kuendeleza maendeleo ya binadamu, elimu na ustahimilivu.”

“Hebu tufanye kazi pamoja, Afrika, Japani, na washirika wetu ambapo teknolojia inaunganisha uhifadhi na maendeleo ya binadamu, kulinda maelewano kati ya watu na sayari.”

Anasema teknolojia inaweza kuwa kiunganishi muhimu kati ya uhifadhi na maendeleo ya binadamu, hivyo kuchangia kulinda maelewano kati ya watu na mazingira wanayoishi.

Aidha, katika hotuba yake, Dr. Chana amepongeza utaalamu wa kiteknolojia kutoka Japani na namna unavyoweza kukamilisha juhudi za uhifadhi barani Afrika, hasa kwa kutumia mbinu shirikishi zinazolenga jamii.

Anasema kwa Tanzania changamoto ya migogoro kati ya binadamu na wanyamapori bado ni kubwa, hususan katika maeneo yanayopakana na hifadhi za taifa, jambo linaloathiri maisha, usalama wa chakula na elimu kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo.

Dr. Chana anasema kuwa utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Uhalifu wa Wanyamapori (WEMS) uliobuniwa na Kikosi Kazi cha LATF na washirika wake, umeimarisha nafasi ya Tanzania katika kupambana na uhalifu wa wanyamapori na misitu katika ukanda wa Afrika.

Mfumo huo unaiwezesha Tanzania kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha juhudi za kikanda za kudhibiti ujangili na biashara haramu ya viumbe hai, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa Lusaka wa mwaka 1994.

Kikosi Kazi cha Mkataba wa Lusaka kinaendelea na mipango ya kuanzisha Kituo cha Kamandi na Udhibiti cha Mkoa, ambacho kitakuwa kitovu cha ukusanyaji wa taarifa, uratibu wa hatua na tathmini ya utekelezaji wa sera dhidi ya uhalifu wa mazingira.

Mkataba wa Lusaka ni mkataba wa kipekee unaoongozwa na Afrika tangu mwaka 1994 kwa lengo la kukuza ushirikiano baina ya nchi wanachama katika kuvunja mitandao ya uhalifu wa kimazingira hasa ule unaovuka mipaka.








# CHAN ILIVYOCHOCHEA UTALII TANZANIA

## KAMPENI YA TINGA CHAN, TINGA TANZANIA – YOU WIN EITHER WAY

Mpira wa miguu unatajwa kuwa mchezo namba moja duniani kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi. Michezo, hususan kandanda, imekuwa daraja la kuwaleta watu pamoja, kukuza amani na mshikamano, lakini kubwa zaidi imekuwa kichocheo cha uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Kwa Tanzania, mpira wa miguu ni zaidi ya mchezo – ni fursa. Shirikisho la Soka Afrika (CAF) lilipoipa Tanzania nafasi ya kuwa mwenyeji mwenza wa michuano ya CHAN 2024 sambamba na Kenya na Uganda, lilikuwa ni uthibitisho wa ukuaji wa soka la Tanzania na pia ubora wa miundombinu na uwezo wa taifa kusimamia matukio makubwa.

Kupitia kampeni ya Tinga Chan, Tinga Tanzania – You Win Either Way, tuliwaonesha wageni kuwa Tanzania si tu mwenyeji wa michuano bali ni nchi bora kwa safari duniani. Wageni walipofika walipata zaidi ya mpira – waligusa historia, wakala vyakula vya asili, walitembea mitaa ya Dar es Salaam, wakaguswa na vivutio vya hifadhi zetu na ukarimu wa Watanzania.





# DAR ES SALAAM NA URITHI WAKE KATIKA UTALII WA MICHEZO

Dar es Salaam kama mwenyeji wa Kundi B lililojumuisha mataifa ya Madagascar, Mauritania, Burkina Faso na Jamhuri ya Afrika ya Kati, ilipata fursa kubwa ya kutangaza vivutio vyake. Takribani watu 120 wakiwemo wachezaji na benchi la ufundi waliweka kambi jijini. Wageni hawa waliondoka na taswira ya jiji lenye historia ya kipekee kuanzia Bandari ya kale ya German Boma, masoko ya kisasa na ya kienyeji, hadi Daraja la Nyerere na la Tanzanite linalounganisha jiji la kisasa na pwani yenye mandhari ya kuvutia.

Kwa namna hiyo, Dar es Salaam iligeuka daraja la michezo na utalii. Uwanja wa Benjamin Mkapa, wenye uwezo wa kuchukua mashabiki 60,000 na ulioboreshwa kwa viwango vya kimataifa, uliwaonyesha wageni uwezo wa Tanzania kuwa mwenyeji wa michuano mikubwa zaidi barani Afrika.






# CHAN NA ATHARI CHANYA KWA SEKTA YA UTALII

## 1. Utalii wa Hoteli na Chakula

Hoteli kubwa kama Johari Rotana, Serena, Hyatt na nyingine zilihudumia timu na mashabiki, huku zikijitangaza kimataifa kupitia mitandao ya kijamii ya mashirikisho ya soka. Wageni walionja vyakula vya asili vya Tanzania kama mishikaki, samaki wa kupaka, wali wa nazi na ugali wa mboga – ladha ambazo ni vivutio vyao kurejea nchini hata baada ya mashindano.

## 2. Miundombinu ya Kisasa

Wageni wa CAF, viongozi na mashabiki waliona kwa macho yao barabara za kisasa, majengo marefu kama PSSSF Tower, na daraja za kisasa zilizolifanya jiji liwe na mvuto wa kitalii. Hii imeongeza imani kuwa Tanzania ni kituo cha michezo na utalii kwa wakati mmoja.

## 3. Ajira na Ushawishi wa Kijamii

CHAN 2024 ilizalisha ajira za muda kwa madereva, wapishi, wahudumu, na watu wa maandalizi ya viwanja. Pamoja na ajira, ilileta mwingiliano wa wageni na wakazi, jambo lililoongeza mzunguko wa fedha na kutengeneza marafiki wapya wa Tanzania.

## 4. Jarida la Wageni

Kama sehemu ya kampeni ya Tinga Tanzania, jarida maalum liliandaliwa na kusambazwa kwa wageni. Jarida hili liliainisha vivutio vya karibu kama Bagamoyo na Kigamboni, mapendekezo ya kutembelea hifadhi za taifa kama Saadani, Mikumi na Nyerere, na ushauri wa sehemu nzuri za malazi. Wageni walipata urahisi wa kuchagua pa kwenda iwe kwa safari ya siku moja au mapumziko marefu zaidi.





## YOU WIN EITHER WAY – TINGA TANZANIA


CHAN 2024 imeonyesha kwamba utalii wa michezo ni nyanja inayoongeza thamani kubwa kwa taifa. Tanzania imetengeneza jina si tu kwa ubora wa soka bali pia kwa vivutio vyake vya kipekee duniani. Wageni walipoingia Tanzania, walishinda kwa kutazama soka na kushuhudia nchi bora ya safari. Watanzania walishinda kwa kupata ajira, kipato na matangazo ya kimataifa.

Kwa hakika, kupitia Tinga Chan, Tinga Tanzania – You Win Either Way, taifa letu limechochea utalii na kujiandaa kwa nafasi kubwa zaidi ya kuwa mwenyeji wa AFCON 2027.


TINGA CHAN,
TINGA TANZANIA
YOU WIN EITHER WAY
5H-AAS
Serengeti
TINGA
tanzania
TANZANIA
Unforgettable!
WWW.TANZANIATOURISM.GO.TZ


Tinga tanzania
TANZANIA
THIS CHAN
Travel the Tanzania
You've Never Seen
TANZANIA
Unforgettable!


TO THE QUARTERS
TANZANIA


TANZANIA




# DKT. CHANA AHIMIZA USHIRIKIANO KATI YA JAPAN NA NCHI ZA AFRIKA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dr. Pindi Chana, ameihimiza Serikali ya Japan kuendeleza ushirikiano na nchi zinazoendelea, kwa lengo la kuongeza ajira kwa vijana na wanawake, kukuza viwanda, kuongeza uzalishaji na kupunguza uhalifu.

Dr. Chana ametoa rai hiyo jijini Yokohama, Japan wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Miji ya Afrika na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) pembezoni mwa Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi na Serikali (TICAD 9).

Anasema huu ni wakati muafaka wa kuimarisha ushirikiano baina ya bara la Afrika na Japan.

Anasema mpango wa kuwa na miji dada kati ya Japan na nchi za Afrika na Asia ni hatua itakayochochea fursa za kujifunza kutoka kwa kila upande na kuimarisha maendeleo endelevu.

"Idadi ya vijana inaongezeka duniani kote na katika nchi nyingi ni asilimia 50 ya idadi ya watu, wanahitaji ajira ili dunia iwe salama na kupunguza uhalifu. Hivyo, kushirikisha vijana katika michezo, kilimo, sayansi na teknolojia kupitia serikali na sekta binafsi ni jambo la msingi," anasema Dk Chana.

Dk Chana ameeleza kuwa Tanzania iko tayari kushirikiana na Japan kwa kuzingatia mikataba ya kimataifa ya Umoja wa Mataifa inayoweka misingi ya ushirikiano wa maendeleo.

“Milango yetu iko wazi. Tanzania inakaribisha mashirikiano yenye manufaa kwa nchi zetu na kwa sayari yetu kwa ujumla.”

Dk Chana ametumia fursa hiyo kuipongeza Serikali ya Japan kwa ushirikiano wake na Tanzania, na kusisitiza umuhimu wa kuwawezesha wanawake na vijana, kuhimiza ubunifu na kufungua milango ya mawazo mapya katika sekta mbalimbali.

“Tunahitaji mageuzi ya kifikra. Tunahitaji kuwa wabunifu, tujifunze kutoka kwa wenzetu, tuwe tayari kubadilika kwa ajili ya vizazi vijavyo.” aliongeza.

Aidha, Dk Chana alibainisha kuwa Tanzania ni nchi yenye fursa nyingi za kilimo, ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa mazao kama pamba, matunda na mboga mboga.

Pia alisisitiza kuwa ni wakati muafaka wa kuuza bidhaa zenye thamani kubwa kwa kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao hayo kupitia viwanda.

Uhusiano kati ya Serikali za Mitaa za Japani na nchi za Afrika umeendelea kuimarika kupitia miradi ya JICA na ushirikiano wa pande mbili, huku TICAD 9 ikitumika kama jukwaa muhimu la kuendeleza mahusiano hayo na kuchochea maendeleo ya kikanda kupitia mtazamo wa ushirikiano wa kimataifa.





# HADITHI YA MILIMA MIWILI: LAKINI UPI NDIO WA TATU KWA UREFU TANZANIA?

Inajulikana wazi kuwa Mlima Kilimanjaro, ulioko Moshi, ndio mrefu zaidi nchini Tanzania.

Kilimanjaro wenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari pia ndio kilele cha juu zaidi barani Afrika.

Watu wengi pia wanafahamu kuwa Mlima Meru unaopatikana Arusha ambao kilele chake kimefika mita 4,562.13 kutoka usawa wa bahari ndio wa pili kwa urefu nchini Tanzania na unashika nafasi ya nne barani Afrika.

Lakini je, ni mlima gani sasa ambao unaweza kuwa unashika nafasi ya tatu kwa urefu nchini Tanzania?

Hii ndio hadithi ya milima miwili, mmoja ni Oldonyo Lengai, maarufu kama 'Mlima wa Mungu,' ulioko wilayani Ngorongoro, na mwingine ni Mlima Hanang' ambao uko karibu na ziwa Balangida, Mkoani Manyara.

Oldonyo Lengai ndio mlima wa pekee wenye volcano iliyo hai, na hakina umekuwa ukilipuka katika vipindi tofauti, mara ya mwisho ikiwa ni mwaka 2007.

Hadi sasa urefu wa Mlima Lengai bado ni kitendawili, maana kuna baadhi wanadai urefu wake ni kati ya mita 2900 hadi 3100 kutoka usawa wa bahari.

Vivyo hivyo kwa mlima Hanang' ambao pia urefu wake unadaiwa kuwa kati ya mita 2800 hadi 3400.

Hata hivyo vipimo kamili vya vilele vya milima hii miwili bado havijabainishwa wazi, kwa hiyo kilichobaki ni ushindani baina ya wakazi wa maeneo yanayoizunguka, kila upande ukidai kuwa mlima wao ndio mrefu zaidi.

Lakini katikati ya mabishano hayo, ghafla umeibuka mlima wa tatu. Huu unaitwa Lolmalasini na unapatikana katika nyanda za juu zilizomo ndani ya hifadhi (Mamlaka) ya Ngorongoro.



Uongozi wa mamlaka hiyo (NCAA) unadai kuwa Lolmalasini ndio hasa mlima wa tatu kwa urefu Tanzania, baada ya Kilimanjao na Meru.

Miaka kadhaa iliyopita, mgeni kutoka ughaibuni, Juan Ramon Morales alisema kuwa yeye amefanikiwa kuupima mlima Lolmalasini wakati alipokuwa akifanya utalii ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Morales anadai kuwa akiwa anafanya utalii wa kutembea kwa miguu, kutokea eneo la Nainokanoka alitumia vipimo vya GPS na kugundua kuwa Lolmalasini una urefu wa mita 3825 kutoka usawa wa bahari na hivyo kuufanya uwe wa tatu kwa urefu Tanzania.

Ikumbukwe kuwa milima yote mitano inayosemekana kuwa mirefu zaidi nchini Tanzania, inapatikana kanda ya kaskazini. Na pengine ndio maana wakazi wa kata ya Tukuyu, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, nao sasa wanadai kuwa Mlima Rungwe ndio unatakiwa kuwa wa Tatu kwa urefu nchini, ingawa vipimo vyake havijabainishwa wazi.

Kutokana na sintofahamu hii kwa sasa kuna haja ya Tanzania kupitia wizara ya Maliasili na Utalii, kufanya vipimo na kuweka hadharani orodha ya milima yote mirefu iliyoko nchini.




Kamati ya Tuzo za Usalama wa Chakula Barani Afrika (African Food Prize Committee. AFP) ikiongozwa na Mwenyekiti wake Rais Mstaafu wa awamu ya nne Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, jumatano Agosti 6 2025 imetembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro baada ya kuhitimisha mkutano wa kamati hiyo uliofanyika Jijini Arusha Agosti 5 katika hoteli ya Gran Melia.









NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula, ametembelea kituo cha utafiti wa nyuki wadogo (Beetopia) kilichopo Ngurudoto, Jiji la Arusha, kinachoendeshwa na Warren L. Steyn na Dkt. Kathrin Krausa.

Kituo hicho hutumika kutoa mafunzo kwa wafugaji wa nyuki wa mikoa ya Arusha na jirani, huku pia kikiwa kivutio cha watalii wa ndani na nje ya nchi wanaopenda kujifunza maisha na tabia za nyuki wadogo.








Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amefungua rasmi onesho maalum la picha katika kuadhimisha miaka 80 ya ushindi wa vita vya upinzani vya watu wa China dhidi ya uvamizi wa Japani na vita vya kupambana na Ufashisti duniani.

Ufunguzi huo umefanyika Agosti 15, 2025 katika Makumbusho ya Taifa la Tanzania jijini Dar es Salaam






Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana ameshiriki katika hafla ya maadhimisho ya miaka 79 ya Uhuru wa India uliofanyika jijini Dar es salaam Agosti 17,2025.





Makamu wa Rais Mhe. Philip Isdor Mpango amekabidhi tuzo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kufuatia utendaji mzuri wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), tuzo ambayo imepokelewa na Naibu Waziri Mhe. Dunstan Kitandula kwa niaba ya Mhe. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii.

Tuzo hiyo imetolewa kwenye ufunguzi rasmi wa Mkutano wa Majadiliano wa Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi za Serikali ulioandaliwa na Msajili wa Hazina katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha





Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amekutana na kufanya mazungumzo na ujumbe kutoka Ubalozi wa Iran nchini Tanzania ukiongozwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni cha Iran, Dkt. Mohsen Maarefi na kujadiliana mashirikiano katika Sekta ya Malikale, Utalii na mafunzo.






Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) imewakabidhi zaidi ya Mizinga 200 ya nyuki kwa Machifu wa Mkoa wa Rukwa ikiwa sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufungaji Nyuki kwa Tanzania iliyo Bora ujulikanao kama 'Achia Shoka Kamata Mzinga'.



# VIVUTIO VIWILI NAMBA 1 VYA DUNIA VINAPOKUTANA: SERENGETI X MARRIOT

## Na Mwandishi Wetu

Loji ya Kifahari ya Mapito Safari Camp itakayoendeshwa kwa ubia kati ya kampuni ya Delaware Investment na kampuni kubwa duniani ya Marriot International imezinduliwa jana Agosti 29, 2025 katika eneo la Robanda, Serengeti nje kidogo ya Hifadhi yenye mvuto duniani: Serengeti.

Huu ni uwekezaji wa brand mbili namba moja duniani, Serengeti ikiwa Hifadhi namba moja Afrika na dunia kwa ukubwa na mchanganyiko murua wa wanyama wengi na moja kwa tukio la wanyama wanaohama na kwa upande mwingine Marriot International, kampuni inayoongoza duniani kwa kumiliki au kusimamia hotels na loji na kwa ujumla ikiwa namba moja duniani kwa kumiliki au kusimamia vyumba vingi vya kulala. Hii inaweza kuitwa "a meeting of two firsts."

Hii inakuwa loji ya kwanza katika maeneo ya karibu ya Hifadhi kwa Marriot kujihusisha nayo hata hivyo haitakuwa ya mwisho hapa Tanzania.

Kutokana na sera nzuri na mvuto wa utalii nchini Tanzania tutarajie jingine kubwa: mwaka 2026 kampuni hiyo pia inatarajiwa kufungua hoteli ya kifahari ya vyumba zaidi ya 30 ya JW Marriot Serengeti Lodge ikiwemo vyumba vya kulala wageni wa hadhi ya juu kabisa (Presidential Suites) viwili inayoendelea kujengwa ndani ya Hifadhi ya Serengeti.

"Mapito Safari Camp will mark a defining moment for Autograph Collection as we introduce the brand's first safari experience in one of the world's most breathtaking wildlife destinations," amepata kusema Jerome Briet, Mtendaji Mwandamizi anayesimamia maendeleo kwa nchi za Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika kutoka kampuni ya Marriott International.




Marriot imejenga au inasimamia kwa ubia au kibiashara zaidi ya maeneo 9,000 ya kulaza wageni iwe hoteli au loji katika nchi 144 na wakifanya kazi kwa muungano wa kibiashara na zaidi ya brand 40 tofauti tofauti.

Huu ni mwendelezo wa sio tu Hifadhi ambazo ni vituo muhimu vya utalii nchini bali destination Tanzania kwa ujumla wake kuendelea kupokea uwekezaji wa makampuni yenye majina makubwa katika utalii kufuatia filamu ya Royal Tour iliyomshirikisha Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akitangaza utalii na vivutio vingine nchini.





# Wageni wa kimataifa waliotembelea Tanzania Januari hadi Julai 2025




Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii